**LEARNING BY EAR 2011**

# “The Promised Land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE TWO: “Different Routes, Same Destination”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI: Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

### SCENE ONE: LINDA BEING INTERVIEWED FOR HER STUDENT VISA

- **Linda (f, 20)**
- **Embassy official (m, 45 - European accent)**
- **Mixed crowd (3-4 people, age and gender not important)**

### SCENE TWO: FARAHANI AND SULE BY THE SHORE

- **Farahani (m,19)**
- **Sule (m, 19)**

**SCENE THREE: LINDA AT HOME WITH HER PARENTS**

- **Linda (f, 20)**
- **Mr. Maraga (m, 60)**
- **Mrs. Maraga (f, 55)**
- **Chivasi (m, 22)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu katika sehemu ya pili ya mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu Wa-Afrika wanaohamia barani Ulaya. Katika sehemu ya kwanza tuligusia maisha ya vijana wanne, Farahani na raiki yake Sule kutoka Afrika Kaskazini mwenye ndoto ya kuishi Ulaya, Chivasi na mpenzi wake Linda ambao ndio mwanzo wamefuzu chuo kikuu, na anayekabiliwa na uamuzi mgumu. Pia tumekutana na Bwana na Bibi Maraga ambao wanatumia akiba yao yote kumpeleka Ulaya binti yao Linda kusomea uanasheria. Je! Nini kitakachojiri. Endelea kuwa nasi katika sehemu hii ya pili “**NJIA TOFAUTI, KITUO KIMOJA”.**Ambapo tunaanza na Linda akifanyiwa mahojiano na maafisa wa ubalozi kabla ya kupewa hati ya Visa.

**SCENE ONE: LINDA BEING INTERVIEWED FOR HER STUDENT VISA**

1. **SFX: OFFICE ATMO, THEN DOOR OPENS**

2. **EMB. OFFICIAL: (calls out)** Bi Linda Maraga!

3. **SFX: MURMURS FROM MIXED CROWD**

4. **EMB. OFFICIAL:** **(calls out again)** Linda Maraga! Kwa mara ya mwisholl!

5. **LINDA:** **(waking up)** Ni mimi!. Samahani niko hapa!

6. **EMB. OFFICIAL:** Bi Maraga, hapa si mkahawani!. Hebu tafadhali nifuate.

7. **SFX: DOOR BEING OPENED AND CLOSED**

8. **LINDA:** Samahani sana kuhusu hilo!.

9. **EMB. OFFICIAL:** **(calm)** Kwani unaumwa Binti Maraga?

10. **LINDA:** Hapana. Ni vile tu mlolongo ni mrefu, ndiposa nikaamua kulala hapa nje ya Ubalozi kidogo nisikose nafasi hii ya mahojiano. Jana sikulala vizuri.

11. **EMB. OFFICIAL:** Idadi ya watu wanatuma maombi ya visa inazidi kuongezeka kila mwaka.Hii ni kazi nyingi sana kwetu. **(changes tone)** Eehe,- kwanini unataka kuhamia nchini mwangu?

12. **LINDA:** **(nervously)** Ku… kusoma .

13. **SFX: FAINT TYPING ON A COMPUTER KEYBOARD ON BACKGROUND**

14. **EMB. OFFICIAL:** Hmm… kusoma. Kusomea nini?

**15. LINDA:** Naenda kusomea uanasheria... maelezo yote yako hapa.

**16. EMB. OFFICIAL:** **(plainly)** Binti Maraga nafahamu vyema kilichoko kwenye faili yako. Jibu tu swali langu!... Kwani huwezi kujiunga na chuo kikuu hapa nchini au vilivyoko nchi nyingine Barani Africa? Gharama ya hapa ni nafuu sana kwako.

**17. LINDA:** Ni kweli, vyuo vikuu viko hapa Barani Africa, lakini si vya hadhi kama vinavyopatikana barani Ulaya. Nikifuzu na shahada ya Digrii kutoka Ulaya, nitakuwa na nafasi nzuri ya kuajiriwa kazi yenye mshahara mzuri!.

**18. EMB. OFFICIAL:** Nani anagharamia masomo na malazi yako?

**19. LINDA:** Wazazi wangu!. Tayari wamelipa karo yote ya muhula wa kwanza!. Kuhusu malazi, nitakodisha katika makaazi ya wanafunzi chuoni humo.

**20. EMB. OFFICIAL:** Masomo yako yatachukua muda wa miaka mitatu, sivyo?

**21. LINDA:** Ndiyo nadhani yatachukua muda huo, kwasababu ni Wazazi wangu wanaonilipia masomo yangu huko ng'ambo!.

**22. EMB. OFFICIAL:** **(sternly)** Unadhani?Bi Maraga,Si mambo ya

kudhania. Nataka unieleze kwa uhakika nani atakaye gharamia malazi yako Ulaya?. Wazazi wako wanafanya kazi gani ?

**23. LINDA:** Wote ni watumishi wa umma.

**24. EMB. OFFICIAL:** Unajua kwa hakika mishahara yao ya Mwezi?

**25. LINDA:** **(puzzled)** Ah… ahh…Sina hakika. Lakini maelezo ya kuhusu mishahara yao …

**26. EMB. OFFICIAL:** Nimekueleza tangu mwanzoni. Kwamba nimepitia faili yako!. Nataka wewe ujibu maswali yangu Bi Maraga. Kwa hivyo hujui wazazi wako wanapokea mishahara kiasi gani?

**27. LINDA:** Kwa heshima yako, suala la mishahara wanayopokea wazazi wangu halinihusu. Sijawahi kuwauliza na wala hawajanieleza.

**28. EMB. OFFICIAL:** Unataka kurejea nchini baada ya kukamilisha masomo yako?

**29. LINDA:** Ndiyo!.

**30. EMB. OFFICIAL:** Nitakuamini vipi kwamba nikikupa visa hutapotelea huko Ulaya?

**31. LINDA:** **(takes a deep breath)** Kwasababu nimeposwa.

**32. EMB. OFFICIAL:** **(changes to happy tone)** Oh, kweli? Pongezi sana! Na harusi ni lini Bi Maraga?

**33. LINDA:** **(tired and exasperated)** Baada ya kukamilisha masomo yangu…. **(pause)** ….

**34. EMB. OFFICIAL:** Vyema kabisa!Ni hayo tu.

**35. LINDA:** **(surprised)** Kwa hivyo…

**36. EMB. OFFICIAL:** Nitakupa Visa Bi Maraga, lakini kwanza unahitajika kulipa ada ya Yuro 60!. Kwa hivyo nenda moja kwa moja hadi kwa keshia na atakupa risiti baada ya kulipa ada hiyo. Kwa mara nyingine pongezi sana kwa kuposwa na nakutakia kila la kheri katika masomo yako.

**37. LINDA:** **(relieved)** Asante sana!

**38. SFX: DOOR OPENS**

**39. NARRATOR:** Ukiuliza Mtu yoyote ambaye amejaribu kutafuta visa ya kwenda Ulaya bila shaka atakuelezea ugumu wake.Maombi mengi hukataliwa lakini kamwe wengi hawaja kata tamaa.Linda ni miongonima watu waliobahatika kupata visa. Na anapoondoka katika ofisi za ubalozi huo akiwa na furaha, kwengineko Africa Kaskazini, Farahani anakutana na rafikiye Sule.

**SCENE TWO: FARAHANI AND SULE BY THE SHORE**

**40. SFX: WAVES GENTLY HITTING THE SHORE**

**41. SULE:** **(in disbelief)** Farahani! Wewe umechanganyikiwa!

**42. FARAHANI:** Sikiliza hapa Sule,Ndio tumaini langu la mwisho. Tutaandamana au la?

**43. SULE:** Ningependa sana lakini na wasi wasi sana. Kwani huogopi Farahani?

**44. FARAHANI:** Kuogopa? Kuogopa nini? Hatuna cha kupoteza hapa, tukifaulu kusafiri faida yake ni kubwa kwetu!

**45. SULE:** Unahakika tutafaulu?

**46. FARAHANI:** Sina hakika, Sule. Lakini kwanza tujaribu!. Tukishindwa basi tutatafuta mbinu nyingine.

**47. SULE:** Basi tutafute njia nyingine. Hii ni unayopendekeza ni hatari sana barahani.

**48. FARAHANI:** Njia nyingine zinajulikana sana!. Ni juzi tu baadhi ya wahamiaji walikamatwa wakiwa kwenye mashua kuelekea Ulaya. Na unajua kilochowapata?

**49. SULE:** Walipigwa risasi.?

**50. FARAHANI:** La hasha hawakupigwa risasi. Si rahisi kuuawa!. Wahamiaji si wahalifu. Huwa tu wanarejeshwa nyumbani.

**51. SULE:** **(realising)** Oh… sasa nimeelewa.Kwa hivyo unataka tujifiche tusionekane kwenye Rada. Wewe ni mwerevu sana. Na sasa familia zetu je?, jamaa, ndungu na maraiki?. Tuwaahamishe?

**52. FARAHANI:** Tutawafahamisha tukifika Ulaya.

**53. SULE:** Na tusipoanikikiwa ,… eeh tusipofanikiwa kufika Ulaya?

**54. FARAHANI:** Tutaendelea kujaribu tu..!

**NARRATOR:** Farahani amevumbua mbinu ya kuingia kisiri barani Ulaya.Lakini anakusudia nini hasa?. Na je atafanikiwa?. Je Sule pia ataandamana naye au atabadili nia? Sakata hii bado inaendelea…… Kwa upande wake Linda amepata Visa yake na sasa amefika nyumbani kuwaonyesha wazazi wake.

**SCENE THREE: LINDA AT HOME WITH PARENTS**

**(Joy, laughter and excitement in the air from the Maraga family)**

**55. MRS. MARAGA:** Ah Linda, Leo nina furaha isiyo na kiafani.

**56. MR. MARAGA:** Pia mimi umenivisha kilemba cha fahari. Hebu nione tena hiyo Visa…….

**57. LINDA:** Baba- tayari umeiona mara nyingi sana…..alah… haya hii hapa!

**58. SFX: PASSPORT PAGES BEING SHUFFLED OPEN**

**59. MR. MARAGA:** **(reads out)** Linda Maraga,Visa ya Mwanafunzi.muda wa kutumika miaka mitatu. ***Multiple entry***. Na hii inamaanisha nini? Kwamba sisi pia tunaweza kuingia Ulaya?

**60. LINDA:** Hapana Baba, hii inamaana kwamba naweza kuingia na kutoka Ulaya wakati wowote visa hii itakuwa ikitumika

**61. MR. MARAGA:** Aha, kumbe. Hatuna bahati!. Sawa lakini Linda!. Tayari nimekukatia tikiti. Utasafiri mwishoni mwa wiki.

**62. LINDA:** **(shocked)** Wikendi hii? Baba bado nina mambo mengi ya kufanya!. Lazima nijiandae, kununua vitu ninavyohitaji, kupanga mizigo yangu na kuwaaga marafiki.…

**63. MR. MARAGA:** Usinilaumu lakini. Hiyo ni mipango ya Mamako!.

**64. MRS. MARAGA:** Samahani lakini lazima tufanya haraka kwani maofsa wa Ubalozi wanaweza kubadili kauli yao. Kwa maelezo uliyotupa wanaweza kubadili nia.

**65. SFX: MOBILE RINGTONE WITH COOL MUSIC**

**66. LINDA:** Samahani kwanza nijibu simu hii faraghani.

**67. MRS. MARAGA:** Bila ya samahani Binti… Musalimie Chivasi, na umweleze aje kututembelea, ni siku nyingi hajafika… **(voice gets quieter)**

**68. SFX: DOOR BEING opened and CLOSED**

**69. LINDA:** **(on phone)** Hello, Chivasi, unaendeleaje ?

**70. CHIVASI:** **(on phone)** Unataka kujua kweli au ni salamu tu?

**71. LINDA:** Kama kawaida yangu nataka kujua hali yako!. Samahani niliondoka ghafla siku ile, Lakini….

**72. CHIVASI:** Usijali Linda!. Hebu niambie, umefanikiwa kupata Visa?.Na rafiki yangu alikuwa ametuma maombi yake ya visa kwenda Ulaya lakini yakakataliwa. Siku hizi mambo ni magumu.

**73. LINDA:** Ni kweli!.Lakini mimi nimepata visa yangu Chivasi.Na wazazi wangu wananiarifu safari ni wikendi hii.

**74. CHIVASI:** **(shocked)** Nini?! Wacha mzaha!. Wikendi hii?. Zimesalia siku chacha sana !.

**75. LINDA:** Nafahamu hilo, Chivasi.Lakini Samahani sana kwani muda huo ni mchache sasa, kuwaaga rafiki tu!.

**76. CHIVASI:** **(trying to be strong)** Hakuna neno Linda! . Nataka

ufahamu kwamba nimefurahi sana kusikia hivyo. Kwa kweli ni fahari kubwa!.

**77. LINDA:** Asante sana, Chivasi.Siamini maneno hayo yanatoka kinywani mwako.

**78. CHIVASI:** **(deep breath)** Kwani inamaana tutaagana hivi?.. kwa simu.?

**79. LINDA:** **(supportive)** Hapana! kwanza Mamangu amekualika nyumbani kwa chakula cha jioni. Na pia ningependa sana kukuona kabla ya kusafiri. Kuna jambo nataka tuzungumze.

**80. CHIVASI:** **(doubtful)** Jambo jema au baya?

**81. LINDA:** **(chuckles)** Mmmm…Jambo jema sana

**82. CHIVASI:** **(sigh of relief)** Phew! Sawa, basi mfahamishe Mamako kwamba nimepokea mualiko wake kwa furaha. Nitakuja Kesho kwa chakula cha jioni, nadhani atanielewa..!

**83. LINDA:** Sawa .Basi tuonane kesho!.

**84. SFX: MOBILE PHONE BEEP AS WHEN CALL DISCONNECTS**

**<u>OUTRO:</u>**

Na mazungumzo hayo kwa njia ya simu baina ya Linda na Chivasi ndipo tunakamilisha sehemu hii ya pili ya mululizo wa mchezo huu wa Redio

kuhusu Uhamiaji katika hadithi. **Ardhi ya Ahadi- Kuhusu Waafrica wanaohamia Ulaya.”.** Sasa Linda amepata visa na tikiti ya kusafiri Ulaya. Lakini nini kinachomsubiri Ulaya? Na ni vipi Chivasi ataweza kukabiliana na maisha baada ya Linda kuondoka? Na je huko Africa Kaskazini Farahani na Sule nao watafanikiwa katika mipango yao ya kuhamia Ulaya kisiri? Pata majibu yote kwenye sehemu ya tatu inayofuata. Kumbuka pia unaweza kukisikiliza tena kipindi hiki kupitia mtandao wetu wa www.dw.de/destinationeurope. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.